# KWA MANENO YAO WENYEWE

## UHAMISISHAJI WA KIJAMII TOFAUTI NA UAJIRI WA WANAFUNZI MABALOZI (MULTICULTURAL OUTREACH & RECRUITMENT, MOR)

"UW ilikuwa shule inayojumuisha kila kitu na haikunifanya nichague masilahi yangu dhidi ya mengine. Nilikuwa na fursa, moyo na mazingira ya shule kubwa-na jamii iliyoshirikiana kwa ukaribu sana."



Julia Jannon-Shields, '21
Santa Clara, CA
Mawasiliano na JMU (jamii, mazingira na upangilio)



Ammara Touch, '21
Kent, WA
Masomo ya Biolojia na Kabila za Marekani



Letauaeletise Hunkin, '23
Spanaway, WA
Masomo ya Kabila za Marekani na sayansi ya jamii

"Jamii yangu ilinipata! Wanafunzi kutoka Muungano wa Wanafunzi wa Polynesia walikuwa wanatembea kwenye chuo kikuu wakati wakuingia shuleni na walinitunza vyema. Sasa, hao ni moja wapo wa marafiki wangu bora zaidi."

"Nilifahamu ya kwanza UW ilikuwa chaguo zuri kwangu kwa sababu jinsi inavyojumuisha kila mtu, jinsi ilivyonikaribisha sio mimi pekee lakini alikaribisha hata familia yangu. Ili karibisha mamangu kwa Kihispania — lugha yake. Sikuhitaji kutafsiri."



Rosario Ocampo, '22
Mt. Vernon, WA
Sayansi ya Siasa na Falsafa



Andy V. Manzano, '23
Palmdale, CA
Usimamizi wa Biashara na Utofauti

"Kwa kweli sikuwa na dhana — au ikiwa — ningeliweza kugharamia masomo yangu ya chuo kikuu. Haya yote yalibadilika wakati ambapo wafanyakazi wema wa MOR walinikabidhi kitabu changu binafsi cha ufadhili wa karo ya chuo.



Mahilet Abraha, '23
Shoreline, WA
Usimamizi wa Rasilimali watu na mifumo ya teknolojia ya habari



Favian Mares, '22
Toppenish, WA
Masomo, jamii na mashirika

"Wakati wa majadaliano na kampuni wahoji wangu wameshanganzwa na kiwango cha uzoefu nilichopata kupitia masomo yangu kwa UW."



Tina Nguyen, '22
Seattle, WA
Teknolojia ya habari na saikolojia



Jordan Crawford (Kuskokwim), '21
Black Diamond, WA
Usimamizi wa Biashara (masoko)


AMINI NDOTO ZAKO.
SISI TUNAAMINI.
W
HUSKIES

# GEUZA NDOTO YAKO KUWA UKWELI

Tunafahamu ya kwamba una ndoto kubwa na tunafanya kazi kwa bidii kuzitekeleza. Wakati unapowaza kuhusu maisha baada ya shule ya upili, tunakukaribisha kujifunza kuhusu Chuo kikuu cha Washington, mahali ambapo ndoto hizi zinatekelezwa.

Kikosi cha Uhamasishaji wa Jamii Tofauti na Uajiri (Multicultural Outreach & Recruitment MOR) kiko hapa kushirikiana na wewe na ni mshangiliaji wako mkuu. Jiunge na washauri wetu wa usajili wa MOR leo. Wako tayari kujibu maswali kuhusu mchakato wa usajili, usaidizi wa kifedha na zaidi. Na pindi tu wewe ni wa Husky, ofisi ya Shughuli za Wachache na Utofauti kinajukumu la kushughulikia mafanikio yako, hadi siku ya kuhitimu.

Tunamsisimko mkuu kuhusu siku zako za usoni -na hatuwezi kugonjea kukufanya UW iwe sehemu ya safari yako. Jiunge nasi.

UNIVERSITY of WASHINGTON

# MULTICULTURAL OUTREACH & RECRUITMENT

Office of Minority Affairs & Diversity

University of Washington
Multicultural Outreach & Recruitment
Box 355845
Seattle, WA 98195

(206) 221-6463

reach@uw.edu

depts.washington.edu/reach

Instagram: @uwmor

Twitter: @uwomadmor

Facebook: @uwmor

**“Kuhudhuria chuo kikuu kutafungua milango ya nafasi ambazo hazijawahi kupatikana kwetu kama familia ya wahamiaji wa mapato duni. Nilikuja UW kwa sababu ilipeana programu nilizokuwa napendelea - na zaidi ya hayo kwa ajili ya msaada wa kifedha.”**



Favian Mares, ’22
Toppenish, WA
Masomo, jamii na mashirika

# KUWA JASIRI KUOTA

## WACHA TUFANYE CHUO KIKUU KUWA RAHISI

Ikiwa kama umeanza kuwaza kuihusu au kama umeshaipata tayari-chuo kikuu cha ndoto yako, tunaelewa ya kwamba kuna changamoto. Kwa hivyo hii ndio ahadi yetu: Mahali popote uliko kwa safari yako, tutakuongoza na kukusaidia ufaulu. Wewe ni mshirika wa UW-na tunataka kukuona hapo.

## UW NI YAKO

Kutoka kwa Puget Sound hadi Spokane, Bellingham hadi Walla Walla na zaidi, UW inajivunia kuwa chuo kikuu cha wanawashingtoni. Mnamo 2020, tulikaribisha idadi ya juu zaidi ya wanachuo wapya kutoka kwa jamii zisizo-wakilishwa sana — ikiwemo wengi kati yao walio wa kwanza kwenye familia zao kuhudhuria chuo kikuu cha miaka nne. Familia yetu kubwa ya Husky iko na nafasi kwako

**29%**

wewe wa Husky kwa UW ni wanafunzi wa chuo kikuu wa kizazi cha kwanza.

**70%**

wanafunzi wa UW wanaajiriwa ndani ya miezi sita baada ya kuhitimu.

# KUKAMILISHA MSTARI

Usaidizi wetu hausiti wakati unapopokea barua ya mwaliko. Wanafunzi wengi kutoka kwa vikundi visivyo wasilishwa vyema wanafuzu kukota kwa chuo kikuu cha UW hapa Settle kuliko chuo kikuu chengine cha umma cha miaka nne katika Washington. Tunafurahia kukutazama umeanza masomo yako na kufanya mabadiliko duniani, na tunataka kuhakikisha ya kwamba kazi yako ya bidii ina manufaa.

*Vikundi ambavyo havija wakilishwa vyema vinajumuisha wanafunzi wa rangi (Mwamerika Mhindi/Mwasili wa Alaska, Mwamerika Mweusi/Mwafrika, Mhispania/Mlatino, Mwasili wa Hawaii/ Mwanakisiwa cha Pasifiki na Mhindi wa Kusini Mashariki) na hata pia wanafunzi kutoka kwa vikundi ambavyo kihistoria vimetekelezwa kutoka kwa masomo ya vyuo vikoo.*

**"Kuna jamii ndogo ndogo nyingi ndani ya chuo kikuu. Nilibahatika kupata yangu kwa urahisi kwa sababu ya programu ambazo UW zinapeana, kwa hivyo kulikuwa na watu ambao nilikuwa ninawafahamu tayari."**



Mahilet Abraha, '23
Shoreline, WA
Usimamizi wa Rasilimali watu na mfumo wa teknolojia ya habari

UNIVERSITY *of* WASHINGTON
MULTICULTURAL OUTREACH & RECRUITMENT
**Office of Minority Affairs & Diversity**

# TUFANYE IWEZEKANE

## MAZUNGUMZO KUHUSU PESA

**HEKAYA:** Ufadhili wa karo ni kwa wanafunzi wanaofaulu mtihani na wanariadha pekee.

**UKWELI:** UW inakaribisha wanaofuzu vyema kabisa na wanariadha wa chuo kikuu — lakina tuna ufadhili wa karo na ruzuku ulioundwa kwa aina yote ya wanafunzi.

**HEKAYA:** Kuhudhuria chuo kikuu inamaanisha kuwa na madeni mengi ya mwanafunzi.

**UKWELI:** Wanafunzi wa UW wanafuzu na kiasi kidogo cha deni kuliko wastani — cha kimataifa na 63% ya UW wa chuo kikuu wanfuzu bila ya deni zinazojulikana.

Kulipia chuo kikuu haipaswi kuwa ghali kupita kiasi. Kutoka kwa ufadhili wa karo na ruzuku hadi nafasi za kufanya kazi kama unasoma, kuna uchaguzi aina nyingi. Washauri wetu wa usaidizi wa kifedha watakusaidia wewe na familia yako kupita mchakato, ili uweze kulipia masomo yako na kufuzu ukiwa na deni kidogo.

**$400 MILIONI**
usaidizi wa kifedha unaopenwa kila mwaka

**#1 CHUO KIKUU**
Inayolipa Zaidi ya

(CNBC Make It)

W

# HUSKY PROMISE YETU

Husky Promise ni uhakikisho wetu kwa wanafunzi wa jimbo la Washington: Hatutawacha changamoto za kifedha zikuzuie kupata shahada ya UW. Ikiwa utahitimu kupokea Husky Promise, ada yako ya chuo kikuu italipiwa yote kikamilifu (ndio-kikamilifu!) kwa miaka nne. Kila mwaka, kadiria wanafunzi 10 000 wa washington hawalipi ada ya chuo kwa UW, ni shukrani kwa Husky Promise. Hii inaweza kuwa wewe.

Jifunze zaidi: **uw.edu/huskypromise**



Jordan Crawford (Kuskokwim), '21
Black Diamond, WA
Usimamizi wa Biashara (mauzo)

**"Nilikuwa mpokezi wa Ufadhili wa Karo wa Costco Diverstity pamoja na Husky Promise na ufadhili zengine zaidi. Rasilimali hizi zilishughuliaka gharama yangu ya kuhudhuria UW- kito ambacho sio cha kawaida kutoka kwa familia inayotesaka kujikimu kimahitaji."**

UNIVERSITY *of* WASHINGTON
MULTICULTURAL OUTREACH & RECRUITMENT
Office of Minority Affairs & Diversity

# PATA FAMILIA YAKO

## SEHEMU UNAPOSTAHILI KUWA

UW sia mahali tu, ni familia. Unaweza kupata watu wenu kwa idadi ya zaidi ya vilabu 1000 vya wanafunzi-kutoka kwa mashirika ya kitamaduni hadi kwa maisha ya Wagriki, mchezo wa mishale hadi kwa uimbaji bila vyombo vya muziki. Chochote kinacho kusisimua, kuna uwezekano wa kupata wengine pia wanaoshiriki shauku yako.

## NYUMBA YAKO YA PILI

Chuo kikuu cha UW ni jamii-na nyumbani kwako ambali na nyumbani. Katikati ya chuo, utapata sehemu zakuvutia, kutoka kwa jumba la makao hadi kwa Samuel E. Kelly Ethnic Cultural Center (kituo kikuu kabisa cha utamaduni kwa taifa) na **wəɫəbʔaltxʷ** – Intellectual House, nyumba yenye muundo mrefu wa sehemu ya mkusanyiko wa wanafunzi wa Wahindi Wamerika na Maasili wa Alaska.

## JAMMI ILIYO PAMOJA NAWE

Hutakuwa pekee yako ukiwa UW. Hata kabla ya kufika hapo, unaweza tegemea washauri ambao wanafahamu ni vipi unavyohisi ukiwa kwa nafasi yako. Ofisi ya Shughuli za Wachache na Utafauti na kikosi cha Uhamasishaji wa Jamii tofauti na Uajiri wanafanya kazi kutengeneza chuo kikuu chenye utofauti, cha kujumisha ambapo kila mtu anaweza kufaulu.

# MWANAFUNZI NA MASHIRIKA YA KITAMADUNI YANAJUMUISHA:

Muungano wa Wanafunzi Weusi

Muungano wa Utetezi wa Wanafunzi Walemavu

Ushirikiano wa Wanafunzi Wafilipini Wamerikani

Mataifa ya Kwanza kwa UW

Ushirikiano wa Mwanafunzi wa Khmer

MEChA de UW

Muugano wa Wanafunzi wa Polynesia

Kikundi cha Zambarau

Watu Tofauti wa Muungano wa Rangi

...na zaidi!

**“Nilikuwa na wasiwasi ya kwamba vyuo vikuu vyengi ni idara za watu weupe sana sana na kuhisi ya kwamba sifai kuwa hapo. Utulivu ulikuja nilipo fahamu ya kwamba sitakuwa pekee yangu, na ya kwamba kuna programu kama Ofisi ya Shughuli za Wachache na Utofauti kusaidia kizazi cha kwanza, wanafunzi wasio wasilishwa vyema.”**



Ammara Touch, ‘21
Kent, WA
Masomo ya Biolojia
na Jamii ya Marekani

UNIVERSITY *of* WASHINGTON
MULTICULTURAL OUTREACH & RECRUITMENT
Office of Minority Affairs & Diversity

UNIVERSITY of WASHINGTON
MULTICULTURAL OUTREACH & RECRUITMENT
Office of Minority Affairs & Diversity


UNIVERSITY of WASHINGTON
MULTICULTURAL OUTREACH & RECRUITMENT
BOX #355845
SEATTLE, WA 98195


FIRST LAST NAME
ADDRESS LINE 1
ADDRESS LINE 2
CITY, STATE ZIP



NDOTO ZAKO ZINAKUITA